Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Sep-2020|
Received: 15.09.2020; Accepted 17.09.2020; Published on 30.09.2020 at www.editoncpublishing.org
Singoei, J. J., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Jinsi Vipengele vya Kitamaduni katika Matini Teule ya Kiswahili na Kikalenjin Vilivyochangia Mtafsiri Kuiandika Upya *Bukuit Ne Tilil*.

**Jane Jepkoech Singoei[1]; Mwanakombo Mohamed [2]; Mosol Kandagor[3]**
**[123]Moi University, Kenya**
**Main author emai: jjbiamah@gmail.com**

## IKISIRI

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza jinsi vipengele vya kitamaduni katika matini teule ya Kiswahili na Kikalenjin vilivyochangia mtafsiri kuiandika upya *Bukuit ne Tilil*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili, ambazo ni nadharia ya tafsiri vitendo ambayo ilitumika kubaini jinsi tofauti za kimazingira kati ya hadhira ya matini asilia na ya matini pokezi ilivyopelekea uandishi upya kufanyika wakati wa kutafsiri. Nadharia ya pili ni ya ulinganifu, ambapo matini asilia ililinganishwa na matini pokezi ili kubaini kama ujumbe ulihifadhiwa katika matini tafsiri. Aidha, tamaduni, matumizi ya msamiati na sarufi zililinganishwa kwa kuchunguza mikakati na mbinu zilizotumika kutafsiri matini asilia, na hivyo kubaini uandishi upya katika matini pokezi. Data zilikusanywa kupitia uchunguzi maktabani na vilevile kuwasaili washikadau katika Ofisi ya Utafsiri wa Bibilia ya Kapsabet na Shirika la Kutafsiri Biblia nchini, pamoja na wazungumza lugha ya Kikalenjin ambao walituelekeza juu ya matumizi ya baadhi ya maneno. Usampuli wa kimakusudi ulitumiwa ili kupata data iliyotumika katika uchanganuzi. Kitabu cha Mithali katika Agano la Kale kiliteuliwa kwa minajili ya utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa: utamaduni wa Waswahili na wa Wakalenjin ni tofauti na hii ilipelekea uandishi upya ufanywe katika tafsiri. Utafiti unapendekeza yafuatayo: Sera za elimu kuhusu lugha za kienyeji zinafaa kutilia maanani tafsiri ya matini za kufundishia.

**Maneno muhimu:** kitamaduni, matini,mtafsiri, *Bukuit ne Tilil*

------------------------------------------------------------------***------------------------------------------------------------------

**How to cite this article in APA (6th Edition)**

Singoei, J.J., Kandagor, Mohamed, M. (2020). Jinsi Vipengele vya Kitamaduni katika Matini Teule ya Kiswahili na Kikalenjin Vilivyochangia Mtafsiri Kuiandika Upya *Bukuit Ne Tilil*. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 2(1), 110-124.

------------------------------------------------------------------***------------------------------------------------------------------



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**UTANGULIZI**

Lugha ni chombo muhimu katika mawasiliano miongoni mwa wanadamu. Kulingana na Ogechi (2002), lugha ni dhana inayotumiwa kurejelea uwezo wa kimaumbile wa akili ya mtu ambao humwezesha kuwasiliana kilugha. Kwa upande mwingine, Shitemi (2001), anasema kwamba lugha ni kifaa muhimu kinachotumiwa na mwanadamu katika mawasiliano. Anataja lugha kama gari la mawasiliano. Hii ina maana kuwa, ufanisi wa mawasiliano baina ya binadamu hutegemea lugha tumizi. Wanadamu wanapowasiliana, ndipo wanapojenga uhusiano wao kama anavyodai

Buliba (2001:54)

> Lugha husaidia sana kuudhibiti uhusiano wa kijamii.....lugha ndiyo huwaleta watu hao pamoja kwa kujenga uhusiano wa kibinafsi katika kiwango cha mtu kwa mtu, mtu kwa jamaa yake, mtu na jamii yake, mtu na taifa lake na mtu na ulimwengu wake.

**Biblia katika lugha ya Kikalenjin**

Kazi ya kutafsiri Biblia ya Kikalenjin ilianzishwa na mmishenari aliyeitwa Stuart M.Bryson, kutokana na haja yake ya kuifikishia jamii ya Wakalenjin imani kumhusu Yesu kristo. Bryson alianzia kazi ya umishenari Kijabe katika chuo cha Biblia cha Moffat baadaye akaenda sehemu ya Kapsabet ambapo alisimamia kituo cha Africa Inland Mission (f). Akiwa Kapsabet, alianzisha shughuli za kutafsiri Biblia katika lahaja moja ya Kikalenjin ambayo ni Kinandi. Alisaidiwa na Mchungaji mmoja kwa jina Rev. Samuel Gimnyige, na wakafaulu kumaliza kazi hii mwaka wa 1939; baada ya miaka kumi (Bryson 1959). Hii ilikuwa Biblia ya kwanza nchini kutafsiriwa katika lugha ya wenyeji wa Kenya. Baadaye, ilibainika kuwa lahaja hii ya Kinandi haikumudu matakwa ya kimawasiliano baina ya Wakalenjin wote kwa sababu ya tofauti za kilahaja. Hapo ndipo walipoanzisha mikakati ya kutafsiri Biblia kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kikalenjin. Kazi hii ilikamilika mwaka wa 1969 chini ya kamati ya wazee wasomi kwa wakati huo (akiwemo hayati rais Toroitich Arap Moi) kutoka lahaja mbalimbali za Kikalenjin, ili kuwezesha watu wa lahaja mbalimbali za kikalenjin kushiriki kwa kutumia Biblia kwa lugha moja.

**Uandishi Upya Katika Tafsiri ya Bibilia**

Biblia ni kitabu kimojawapo cha vitabu vitakatifu ulimwenguni. Hiki ni kitabu mashuhuri chenye misingi ya imani ya Kikristo, na ambacho kinaaminika kubeba mawasiliano maalumu kutoka kwa Mungu hadi kwa binadamu. Hii ndio sababu kitabu hiki kinajulikana kuwa kikongwe sana ulimwenguni. Mungu alipomuumba mwanadamu, moja kwa moja, alianza kuwasiliana naye. Maandishi ya kwanza ya Biblia yalitekelezwa na Mungu mwenyewe pale ambapo aliandika amri kumi na kumpatia Musa ili awape wana wa Israeli (Biblia: Kutoka 20:1-17). Baadaye, Musa alirudia kuziandika amri zile kwa sababu alikuwa ameziharibu zile zilizoandikwa na Mungu mwenyewe. Kuanzia hapo, vitabu vingi vya Biblia viliendelea kuandikwa na watu mbalimbali wakiongozwa na uwezo wa Mungu; kama vile manabii Isaiah, Ezekieli, Amosi, Ezra na wengine, waliojumuika kuandika Agano la Kale. Baada ya Yesu Kristo kuja na kuondoka ulimwenguni, mitume waliandika sehemu ya pili ya Biblia mashuhuri kama Agano Jipya; wengi wa waandishi hawa wakitoa ushuhuda wa kazi zake Yesu akiwa ulimwenguni, pamoja na shuhuda za watu waliomjua Yesu Kristo baada ya yeye kuondoka duniani, kama vile barua zake Paulo.

Kwa hivyo, ni kweli kuwa Biblia ni kitabu kitakatifu, na kinachoaminika kubeba ujumbe wa mwenyezi Mungu kwa wanadamu. Hii ina maana kuwa mtafsiri anapotekeleza kazi yake, anafaa kuzingatia kuhifadhi ujumbe uliyomo kwa makini sana kwa kuzingatia onyo hili.

> "Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

> mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki" (Biblia: Ufunuo wa Yohana 22:18-19)

Wataalamu kama vile Catford (1965), Nida na Taber (1969), Toury (2012), Pym (1995) na Biamah (2012) wanadahili kuwa tafsiri inahusu ulinganifu wa ujumbe wa matini asilia na matini pokezi; kwamba mtafsiri ana jukumu kuu la kuhakikisha kuwa yaliyomo kwenye matini tafsiri ni yale yaliyomo kwenye matini asilia. Ulinganifu huu wakati mwingi hubainika kuwa tata mno kwa kuwa ni vigumu kuwa na lugha mbili zinazofanana au kuafikiana kimuundo na hata kimtindo. Isitoshe, wakati mwingi tamaduni huweza kutofautiana baina ya lugha ya matini asilia na matini pokezi. Mtafsiri katika hali kama hii, atajipata akiandika kazi ile upya tena.

Kila lugha huwa na muundo wake bainifu na ili kuwasiliana kikamilifu, ni lazima kaida za lugha hiyo zifuatwe. Kwa mfano, kila lugha ina muundo wake wa virai, vishazi na sentensi. Ili kufanikisha tafsiri, lazima mtafsiri azingatie muundo wa lugha lengwa; vilevile uteuzi wa maneno na msamiati unafaa kuzingatiwa ili kutekeleza tafsiri kamilifu. Lugha nyingine huweza kuwa na hali ambapo neno huwa na zaidi ya maana moja. Mtafsiri hivyo anastahili kufanya uchunguzi zaidi kuhusu muktadha wa kimatumizi wa neno husika kabla ya kuamua kulitumia. Hii ina maana kuwa atakuwa anaandika upya neno hilo.

Hatim na Mason (1994), Newmark (1988) na wataalamu wengine wa tafsiri wameeleza kuwa ili kutafsiri, mtafsiri lazima ateue mbinu mwafaka za kutumia ili kufanikisha kazi yake. Ujumbe wa mwandishi wa matini asilia hufanikiwa kutegemea mbinu anazotumia mtafsiri. Mbinu hufanikisha au kutofanikisha mawasiliano. Ili mawasiliano yafaulu, itagharimu mwasilishaji wa ujumbe (mtafsiri) kuchukua jukumu la kuteua njia mwafaka ya kutumia ili kuwasiliana na hadhira pokezi kama alivyofanikiwa mwandishi asilia katika hadhira yake. Ili kutafsiri Biblia, mtafsiri atachagua mbinu mwafaka ilmuradi aweze kupitisha ujumbe kwa namna itakavyoeleweka kwa hadhira pokezi. Kwa kuwa lugha mbili haziwezi kuwa sawa, mbinu za kutafsiri huweza kuchangia kazi tafsiri iwe ni uandishi upya. Biblia imetafsiriwa kwa lugha nyingi duniani. Hivyo, kuna uwezekano kuwa ikiwa mbinu za kutafsiri zilizotumika katika tafsiri hizo ni tofauti na zile za Biblia ya kwanza, ina maana kuwa kuna uandishi mwingi mpya wa Biblia ulimwenguni.

Lengo kuu la kuandika Biblia ni kupitisha ujumbe wa Mungu kwa watu wote ulimwenguni na pia vizazi vijavyo. Biblia iliandikwa mwanzoni kwa kutumia lugha za Kihebrania, Kiaramiki na Kigiriki. Baadaye, ujumbe haukuweza kufikia watu wasiokuwa wazungumza lugha hizi tatu. Upungufu huu ulipelekea kuwepo na haja ya tafsiri zaidi. Tafsiri ingehakikisha kuwa watu wote wanapata ujumbe wa Mungu, kama alivyokusudia. Hii ilipelekea kubuniwa kwa mikakati ya kutafsiri Biblia aghalabu katika lugha zote ulimwenguni. Mtindo wa kiuandishi huweza kutofautiana baina ya lugha asilia na lugha pokezi, hasa ikizingatiwa kuwa mwandishi wa matini asilia (M.A) Biblia ya Kiswahili ni tofauti na mtafsiri wa matini pokezi (M.P)- Biblia ya lugha ya Kikalenjin (*Bukuit Ne Tilil*).

Isitoshe, hadhira ya matini ya lugha ya Kiswahili ni tofauti na hadhira ya matini ya lugha ya Kikalenjin; wao wana utamaduni tofauti na falsafa zao ni tofauti kabisa; hasa kutokana na tofauti za kimazingira. Hali hii humlazimu mtafsiri kujikwamua kwayo ili kuifikia hadhira yake kwa njia ambayo kazi yake haitaonekana kuwa ni kazi tafsiri ila kazi asilia na yenye kuafiki hadhira lengwa. Ili kufaulu,



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

mtafsiri aliandika upya M.P. Tafsiri ni kitendo kinachoongozwa na mfumo pamoja na itikadi zilizopo katika jamii husika. Kwa kuwa itikadi na mifumo ya jamii husika ni tofauti, utafiti huu ulichunguza namna mtafsiri alivyofaulu kupitisha ujumbe wa mwandishi asilia. Huku akizingatia tofauti hizi.

Utafiti huu umelenga kuchanganua uandishi upya wa Biblia ya Kikalenjin (*Bukuit Ne Tilil*) kama unavyobainika katika tafsiri yake. Biblia hii ilitafsiriwa kutoka kwa lugha ya Kiswahili katika miaka ya sitini. Lugha ya Kiswahili na Kikalenjin ni tofauti kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu huku Kikalenjin ikiwa ni lugha ya Kinailoti. Hii ina maana kuwa lugha hizi mbili zimetofautiana kisemantiki, kisintaksia, kifonetiki na kadhalika. Isitoshe, Wakalenjin wanaishi sehemu za Bonde la Ufa huku Waswahili wakiishi pwani.

Mazingira kwa kawaida yanachangia kwa wanadamu kujihusisha na shughuli mahsusi ili kujiendeleza kijamii na kiuchumi. Shughuli hizi ndizo zinazozalisha tamaduni zinazopelekea lugha kutofautiana. Kutokana na ukweli huu, ndipo lugha ya Kiswahili inatofautiana na lugha ya Kikalenjin. Wakati wa kutafsiri, mtafsiri anafaa kuangazia tofauti hizi ili kumudu tafsiri yake. Biblia Takatifu iliandikwa kwa lugha ya Kiswahili ikiwalenga Waswahili. Mtafsiri wa lugha ya Kikalenjin anafaa kuzingatia kuwa anaowatafsiria, ambao ni Wakalenjin, wana mila na tamaduni tofauti na za Waswahili. Katika kutafsiri, atalazimika kuandika upya M.P kwa namna itakavyoeleweka kwa Wakalenjin na kuafikiana na mila na desturi zao. Ni kwa misingi hii ambapo utafiti huu umefanywa ili kuchunguza uandishi upya katika tafsiri ya *Bukuit Ne Tilil.*

## MAPITIO YA MAANDISHI

Utamaduni ni mchanganyiko wa kaida za jamii, elimu, sanaa, sheria, itikadi na tabia anazozipokea mwanajamii (Katan, 1999). Utamaduni hubadilika kiwakati. Kadri muda unavyopita ndivyo dhana ya utamaduni inavyobadilika ubongoni mwa binadamu.
Mwanzoni, utamaduni ulikuwa sahili; yaani jinsi maisha yalivyoendelea kisanaa, kielimu na kadhalika. Lakini wakati maana ya pili kuhusu maisha ya watu ilipojumuishwa kwenye ufafanuzi wa utamaduni, hapo ndipo tamaduni nyingine zilipotengwa, nyingine zikawa bora na nyingine dhaifu. Kadri maendeleo ya kisosholojia na stadi za kitamaduni yalivyozidi, ndipo maana ya tatu ya utamaduni ikawa inahusiana na uwezo wa jamii na itikadi. Utamaduni hupatikana katika lugha. Mtafsiri anapotafsiri, atajikuta akihamisha vipengele vya kitamaduni vya L.A hadi kwa L.P kwa sababu hivi viwili havitenganishwi. Matini ya lugha pokezi bila shaka itakuwa na elementi za kitamaduni ya L.A na kuifanya matini hii kuwa na tamaduni mbili iliyochanganyikana, yaani utamaduni wa L.A na wa L.P.

Utamaduni ni hali ya maisha ya mtu katika jamii; iwe ni dini, tabia, mfumo wa elimu na vilevile familia. Inavyoishi jamii moja na kuchukulia maisha, huenda ikawa tofauti kabisa na jamii nyingine. Kwa kuwa tafsiri huhusu lugha mbili na tamaduni mbili kama anavyodai Toury (1978), basi inakuwa ni bayana kuwa mtafsiri hawezi kutenganisha tafsiri na utamaduni. Pym (2000) anaunga mkono dai kuwa tafsiri ni kitendo cha kitamaduni kwa kusema kuwa: Kuangalia tafsiri ni kama kujihusha moja kwa moja na uhusiano baina ya Tamaduni (FY).

Mtafsiri anapotafsiri, hulazimika kuzingatia na kukabiliana na tamaduni mbili:
i) Kukuza utamaduni wa hadhira asilia
ii) Kubadilisha utamaduni asilia
iii) Kuchanganya i na ii



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Hivyo kulingana na Al-Hassan, hali ya pili ndiyo huitwa tafsiri ya utamaduni ila watafsiri huchanganya zote mbili. Katika utafiti huu, tulinuia kuchunguza jinsi watafsiri wa Biblia ya Kikalenjin walivyoishughulikia matini tafsiri kwa kuwa hadhira asilia na pokezi zina tamaduni tofauti na kuwa watafsiri walikusudia kuifikia hadhira pokezi kwa namna ya uwazi na yenye kueleweka barabara. Metini za kifasihi ni mbili. Kwanza ni matini ya kisayansi. Hii aliiainisha kama matini yenye utamaduni jumuishi (universal culture), ambapo kwayo, mtafsiri huitafsiri pweke bila kuzingatia tamaduni mahsusi ila anazingatia tu yaliyomo anapotafsiri bila kuzingatia muktadha wa kitamaduni. Katika kutafsiri matini aina hii, muktadha wa hadhira pokezi na hadhira asilia huchukuliwa kuwa sawa.

Aina ya pili ni ile aliyoiita tafsiri ya kibiashara au matangazo. Aina hii uhusu utamaduni mahsusi na kwa kawaida, haiwezekani kuitafsiri. Badala yake, huandikwa upya katika lugha ngeni ili iweze kufidia tamaduni za lugha ngeni au pokezi. Biblia huweza kuainishwa kama matini ya kisayansi kwa kuwa ni matini yenye hadhira kubwa sana duniani na hadhira hii, huwa na tamaduni mbalimbali. Utafiti wetu ulichunguza jinsi mtafsiri alivyomudu kutafsiri matini hii kwani utamaduni wa Wakalenjin ni tofauti na wa Waswahili. Isitoshe, ilichunguza jinsi tofauti za kitamaduni zilivyosababisha uandishi upya kwa Biblia ya Kikalenjin (*Bukuit Ne Tilil*).

Lugha na utamaduni ni vipengele viwili vinavyoingiliana. Wakati wa kutafsiri, mara nyingi lugha pokezi huweza kubadilika kutokana na ongezeko la vipengele vya kitamaduni kutoka kwa M.A. Matokeo yake ni M.P yenye mchanganyiko wa utamaduni wa M.A na M.P. Isitoshe, mtafsiri hutafsiri ujumbe pamoja na mtindo wa M.A na kuzalisha matini iliyoandikwa upya. Polepole, vipengele hivi vya kigeni huunganishwa na L.P pamoja na utamaduni pokezi na matokeo yake ni mchanganyiko wa vipengele vya M.A na M.P.

Utamaduni ni kipengele muhimu sana katika tafsiri. Mtafsiri anastahili kumudu tamaduni asilia na pokezi ili kufanikisha azma kuu ya tafsiri ya kupanua (enrich) isimu na utamaduni wa L.P. Kwenye utafiti wake kuhusu changamoto zinazosababishwa na tofauti za kitamaduni, Guerra (2012) alibaini kuwa wakati wowote ambapo tamaduni mbili zinapokabiliana, inakuwa vigumu sana kwa mtafsiri kufanikisha uhamisho wa maana ili kufaulu katika jukumu lake la kuwasiliana na hadhira pokezi. Newmark (1988) alibaini hali hii katika utafiti wake wa awali ambapo aliainisha matatizo haya ya kitamaduni kama yafuatayo: Kwanza ni tofauti za kiekolojia.

Ekolojia kwa mujibu wa mtaalamu huyu inahusu tofauti inayotokana na mazingira kama mimea, wanyama, hali ya anga n.k. Ikiwa jamii mbili husika zinapatikana katika mazingira mbali kimasafa, kutakuwa na uwezekano kuwa wanajamii hao watakuwa na welewa tofauti kuhusu ekolojia yao. Hii ina maana kuwa, mtafsiri atakuwa na kazi nzito ya kujaribu kusawiri mazingira yaliyozungumziwa na mwandishi wa matini asilia kwa namna itakayopelekea M.P kuwa na uhalisia kwa hadhira pokezi. Kile kinachopatikana katika mazingira ya wanajamii moja huweza kukosekana katika mazingira ya wanajamii wengine. Kwa mfano, wanyama wanaofugwa na Wakalenjin huweza kuwa tofauti na wanaofugwa na Waswahili. Isitoshe, sababu za kuwafuga mifugo hao huwa tofauti kati ya wanajamii. Hali hii huzua changamoto kwa watafsiri. Jambo la pili ni nyenzo za kitamaduni (material culture). Haya yanahusu mavazi ya wanajamii, vyakula, majina ya miji n.k. Kawaida, mavazi ya Waswahili na Wakalenjin pamoja na vyakula vyao ni tofauti kabisa. Mtafsiri akizingatia tofauti hizi, huweza kujikuta kuwa anapata changamoto kwenye tafsiri yake.

Majina ya watu na miji huwa pia changamoto kwa kuwa licha ya mtafsiri kutaka kuzingatia sintakasia ya L.P, ana jukumu la kuhakikisha kuwa hapotezi maana na dhana



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

iliyozingatiwa na L.A katika kutumia majina husika. Mwisho ni tabia ya wanajamii. Hii inahusu jinsi wanavyoishi, shughuli zao za kujipatia riziki na namna ya kustaarabu kwao. Vilevile kuna miundo ya imani ya wanajamii, mifanyiko ya kisiasa na mamlaka. Utafiti huu ulichunguza matini ya kidini ili kubaini iwapo mtafsiri alikumbwa na changamoto hizi alizozitaja Newmark na kuonyesha namna alivyozikabiliana nazo katika tafsiri ya Biblia ya Kikalenjin.

Tafsiri sio kubadilisha maana wala kubadilisha msimbo bali ni kusafirisha maana kutoka L.A hadi L.P (Snell-Hornby, 1989). Kazi ya mtafsiri ni kuwezesha uhamishaji wa maana na vipengele vya kitamaduni kutoka lugha moja hadi nyingine huku akihakikisha kuwa athari sawa na ile iliyopokewa na hadhira asilia inapitishwa kwa hadhira pokezi. Ujumbe uliopo kwenye L.A kwa kweli huwa umefumwa kwenye muktadha wa kitamaduni na inafaa kuhamishwa hadi kwa L.P (Nida, 1964). Uhamishaji huu unapotekelezwa, ni jukumu la mtafsiri kuhakikisha kuwa ujumbe unahifadhiwa lakini kwa kuegemea muktadha na utamaduni wa L.P.

Newmark (1988) na Agar (1994) katika fafanuzi zao, wanadai kuwa utamaduni ni maisha na mambo ya muhimu na ya pekee katika jamii husika inayotumia lugha kama njia ya kujieleza, na kuifanya jamii hiyo kujihisi kuwa tofauti. Larson (1984) anaona kuwa utamaduni ni mchanganyiko wa Imani, mielekeo, kaida na maadili ambayo wanakikundi hushiriki kwayo. Upekee wa Wakalenjin hutokana na lugha yao ambapo mtafsiri anastahili kutilia maanani ili kuhakikisha kuwa anakuza vipengele vya kitamaduni kama wanavyodai Newmark (1988), Agar (1994) na Larson (1984). Katika Biblia ya Kikalenjin, lugha inayotumika ni lugha inayostahili kuwasiliana na wanajamii ambao wanajitambulisha na lugha yao ya Kikalenjin, kwa hiyo, utamaduni wao lazima uwepo ili mawasiliano yakamilike. Utafiti huu ulichunguza mawazo ya wataalamu hawa yalivyozingatiwa na mtafsiri ili kuhakikisha kuwa utamaduni wa Wakalenjin unazingatiwa katika kupitisha ujumbe wa M.A hadi kwa H.P hata kama kutakuwa na uandishi upya kwenye matini pokezi.

Wataalamu Alvarez na Vidal (1996) wanaeleza kuwa tafsiri hudhihirisha uwezo wa utamaduni mmoja dhidi ya mwingine. Tafsiri si kuzalisha matini inayolingana na nyingine bali ni mchakato changamano wa kuandika upya matini pokezi iliyo sambamba na matini asilia na yenye athari zake tofauti na za matini asilia. Utafiti hata hivyo hautaweza kubaini athari ya matini pokezi kwa wasomaji wake, lakini uchunguzi huu uliazimia kuangalia vipengele ambavyo vinaaminika kuchangia kwa matini kuwa ni uandishi upya wala si tafsiri.

Kila jamii huwa na namna ambavyo huitazama dunia yake. Katika juhudi ya kuunganisha thamani ya lugha na utamaduni, tafsiri wakati wote hujaribu kusawazisha tamaduni tofauti ili kufikia kiwango kinachoeleweka kwa msomaji wa tafsiri (Lefevere, 1999). Hivyo basi, tafsiri hailingani na matini asilia sawa na anavyosema Bassnett (1980) kuwa: matini tafsiri ni tofauti sana na matini asilia na hivyo inafaa kuchukuliwa kama matini ya kipekee. Kama huu utachukuliwa kama ukweli, basi itakuwa dhahiri kuwa kamwe hakuna kazi tafsiri. Tunavyojua ni kuwa Biblia ya Kikalenjin ni tafsiri kutoka kwa Biblia ya Kiswahili. Vipi basi tutaiita uandishi upya wala si tafsiri? Matokeo ya utafiti huu yataweza kutupa mwanga kuhusiana na madai ya Bassnett. Mtafsiri ana kibarua kigumu katika kutoa tafsiri kwa kuwa changamoto ya tofauti za kitamaduni ni dhana nzima yenye vizingiti vyake.

Tuliangalia jinsi mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin alivyofaulu katika utafsiri wake. Hongwei (1999) anatoa maoni yake kuhusu utamaduni kwa kudahili kuwa lugha hutumika



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

kuchora taswira ya utamaduni wa jamii husika. Kulingana naye, lugha ina umuhimu mkubwa ikilinganishwa na vipengele vingine vya kitamaduni kwa kuwa hufanya kazi ya kueneza, kukuza na kuimarisha vipengele vile vingine vya kitamaduni. Dai hili linaelekea kuunga mkono maoni yake Sapir (1949) katika tasnifu yake ya *Language Race and Culture,* ambapo anabaini kuwa lugha haiwi ila kutokana na utamaduni. Hata hivyo, Newmark (1988) anaonekana kupinga Hongwei na Sapir kuhusiana na wazo hili kuwa lugha ni kipengele cha utamaduni, kwa kudai kuwa ingekuwa hivyo, tafsiri kamwe haingewezekana. Lakini tunaona tafsiri ya Biblia ya Kikalenjin inawezekana. Kuhusu uhusiano wa lugha na utamaduni, Kramsch (1998) anaona lugha kama mfumo wa ishara yenye maadili ya kitamaduni. Wazungumzaji hutambulisha utamaduni wao kwa wenzao kupitia lugha. Huona lugha yao kama ishara ya kujitambulisha kijamii, na kutotumia lugha huchukuliwa na wazungumzaji kama uasi dhidi ya wanajamii na utamaduni wao. Hii ndio sababu lugha ni kitambulisho cha jamii. Nida (1964) anadahili kwamba tofauti baina ya tamaduni husababishwa changamoto kubwa kwa mtafsiri kuliko ilivyo tofauti za kimuundo. Katika utafiti huu, tulinuia kuchunguza mikakati inayotumiwa na mtafisiri katika tafsiri ya *Bukuit Ne Tilil* ili kukabiliana na chngamoto hizi. Halafu tukabaini jinsi mikakati hii inavyopelekea uandishi upya wa Bibilia ya Kikalenjin.

Tafsiri nzuri ni ile inayotimiza makusudi sawa katika L.P kama ilivyo katika L.A. Lazima M.P ionekane kama kazi asilia. Ni sharti kazi tafsiri ionyeshe uhalisia wa L.A katika L.P kwa kuzingatia mtindo wa L.A na kuwa na athari ileile kwa H.P. Suluhisho la mambo haya ni kiwango cha usambamba wa ulinganifu. Nida (1964) akizungumzia kuhusu jinsi ya kukabiliana na dhana za kitamaduni endapo kisawe hakipatikani, anapendekeza kuwa mtafsiri huweza kutumia faharasa na tanbihi ili kuelezea dhana za kitamaduni kwa uwazi. Katika utafiti wetu, tulijishughulisha na kuchunguza jinsi mtafsiri wa Bibilia ya Kikalenjin alivyokabiliana na tafsiri ya dhana za kitamaduni.

Salehi (2012) andai kuwa matini hufasiriwa sio kwenye ombwe tupu bali kwa kuegemea kaida za jamii husika ambamo wanajamii huzifafanulia tabia zao na za wenzao. Kaida za kitamaduni huzua changamoto kwa watafsiri na hivyo kuwalazimu kufahamu kwanza tamaduni pokezi kando na tamaduni asilia. Lazima pia atumie mikakati bora zaidi ili kuletea athari sawa. Athari ya kazi tafsiri iliyofaulu ni ile yenye kufanana kwa wasomaji wa L.P kama ilivyo kwa wasomaji wa L.A (Munday, 2001). Kama alivyopendekeza Munday kuhusu matumizi ya mikakati bora katika tafsiri, utafiti wetu ulibaini mikakati hiyo, na kisha kutambua iwapo kulikuwa na uandishi upya wa Bibilia ya Kikalenjin katika harakati ya kutafsiri. Isitoshe, tulichunguza jinsi mtafsiri alivyozingatia kaida za tamaduni ya Wakalenjin katika tafsiri yake kama anavyodai Salehi.

Kuhusu mwingiliano wa tafsiri na utamaduni, House (2009) anasema kuwa tafsiri sio tu tendo la kiisimu bali pia la kitamaduni; ni kitendo cha kuwasiliana baina ya tamaduni. Tafsiri kwa kawaida uhusu lugha na tamaduni kwa kuwa haviwezi kutenganishwa. Lugha imo ndani ya utamaduni, kwa kuwa hueleweka zaidi inapoelezwa ndani ya utamaduni. Mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin anapotafsiri, ana la ziada ili kutumia lugha ya Kikalenjin kudhihirisha utamaduni wa Kikalenjin. Utafiti huu ulichunguza ufanisi wa mtafsiri katika utekelezaji huu.

Baker (1992) anaelezea kuwa neno katika L.A huweza kuwasilisha dhana iliyo tofauti kabisa katika utamaduni wa L.P. Kwa mfano, mambo yanayohusu dini na imani, itikadi na aina ya vyakula na mengine, hukosa visawe katika lugha nyingi. Mtafsiri huweza kusuluhisha tatizo hili kwa kutumia neno lenye kulete athari sawa kwa H.P



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

sawa na ilivyo kwa H.A. Hapo, M.P itaonekana ikiwa sawa na M.A. Utafiti huu ulilenga kuchunguza mikakati iliyotumika katika uteuzi na mpangilio wa maneno katika *Bukuit Ne Tilil,* na kuangalia iwapo uteuzi huo unaleta athari sawa na ile ya Biblia Takatifu. Athari sawa inapopatikana katika ujumbe uliotafsiriwa, husababisha matini hiyo iwe tafsiri ya kuaminika. Dhana ya uaminifu imechambuliwa kwa kina na Shitemi (1997) akitafiti kuhusu dhana hii ya uaminifu katika tafsiri ya mashairi ya kale, anadahili kuwa ukosefu wa habari za kimsingi kwa mtafsiri, huweza kuchangia kuwepo kwa pengo linaloathiri utimizaji wa tafsiri hasa pale ambapo tamaduni na mazingira yanayorejelewa hayana uhusiano wowote wa kiisimu, kimazingira na kitamaduni na ile ya matini pokezi.

Katika utafiti wake Sun (2011), alibaini kuwa kuwepo kwa angalau uwiano wa kiasi fulani baini ya tamaduni, huchangia katika kuwezekana kwa tafsiri baina ya tamaduni. Utamaduni wa Wakalenjin na wa Waswahili huenda ukawa na uwiano wa kiwango fulani, uliosababisha kuwezekana kwa mawasiliano, la sivyo, tafsiri ya Biblia ya Kikalenjin haingewezekana. Waswahili na Wakalenjin ni watu wanaoshi katika taifa moja, chini ya utawala mmoja na siasa sawa, ingawa wametengana kimasafa. Uwiano huu wa utaifa unaosababisha mazingira sawa ya kisiasa, ndio Sun (2011) anadai kuwa humwezesha mtafsiri kufanikisha kazi yake.

Utamaduni vilevile, kama anavyoshikilia Sun (2011) ni kwamba huweza kuwa na maadili yasiyokubaliana kuhusu dhana fulani. Kwa mfano, katika jamii ya Waswahili, paka huweza kuhusishwa na bahati mbaya, huku Wakalenjin wakimchukulia paka tu kama mnyama anayehusishwa na utulivu. Katika kutafsiri dhana za kitamaduni, mtafsiri huenda akajikuta akirejelea dhana ileile kwa namna tofauti na ilivyokusudiwa na mwandishi wa M.A. Upotovu huu huchangia mara nyingi kwa M.P kuandikwa upya, na kuonekana kama ni matini tofauti na ile ya awali. Utafiti wetu ulichunguza jinsi dhana ya utamaduni ulivyoshughulikiwa na mtafsiri wa *Bukuit Ne Tilil.* Vilevile, kutathmini namna alivyoikabili ili kuhakikisha kuwa tafsiri hiyo inafaulu kupitisha ujumbe uliomo kwenye Biblia Takatifu.

## MATOKEO

### Utamaduni wa Wakalenjin

Jamii ya Wakalenjin wana desturi na mila zao zinazoakisi maisha na imani yao ya kila siku, na hutumia lugha kama njia mojawapo ya kipitisha utamaduni wao kutoka kizazi hadi kingine. Katika utafiti huu, tuligundua kuwa vipengele vya utamaduni wa wakalenjin vilibainika katika tafsiri ya Biblia ya Kikalenjin. Mtafsiri katika kuvishughulikia vipengele hivi, ama alifaulu au kupungukiwa katika kuzitafsiri dhana mbalimbali. Hii ilipelekea mtafiti kuchunguza vipengele hivyo, hasa vile vilivyoonekana kupelekea tafsiri isikamilike na hiyo kusababisha uandishi upya wa M.T. Vipengele vilivyobainika kutokana na utafiti huu ni kama vifuatavyo;

### Tafsiri Inayohusu Vyakula

Wakalenjin ni jamii inayofuga wanyama mbalimbali, hasa ng’ombe huchukuliwa kama aina ya mifugo ambayo Mkalenjin halisi lazima awe nao. Ukweli huu unatokana na jinsi Wakalenjin hutumia mifugo hawa kwa kutolea mahari kwa wake wao. Vilevile, wakati wa sherehe zao mbalimbali, wao huchinja ng’ombe. Katika kutafsiri Biblia ya Kikalenjin, ukweli huu unabainika wakati mtafsiri anapotafsiri nyama kwa kusisitiza kuwa ni nyama ya ng’ombe wala si nyama yoyote tu. Tazama tafsiri ifuatayo;

**Mfano 1.**

Mithali 9:2 **M.A -** Amechinja nyama zake, Umechanganya divai yake, Ameiandalia Meza yake pia.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

**Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)**

**ISSN: 2663-9289**

**Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|**
**Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org**
**Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*,** *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**M.P**- *Kigoeny tukyik: kigoburuch divaikyik; kigichob amitwogik eng' mesennyi.*

Katika M.P, mtafsiri anapotumia neno ***tukyik*** (Ng'ombe wake), anatupilia mbali ile
dhana ya ***nyama*** iliyowasilishwa na M.A, na badala yake, nyama yenyewe inafafanuliwa katika M.P kuwa ni ya ng'ombe wala si nyama yoyote tu. Mtafsiri anachagua tafsiri hii kimakusudi ili kupelekea Wakalenjin kuelewa vyema na kuifanya M.P kuwa na athari sawa na ile ya M.A. Katika jamii ya Waswahili, dhana ya nyama inaeleweka kwa wanajamii, ila kwa Wakalenjin, dhana hiyo inalinganishwa moja kwa moja na nyama inayotokana na ng'ombe. Kwani, wao ni wafugaji na ni rahisi kumzungumzia mnyama anayeeleweka kwa wanajamii kwa jumla.
Mkate kwa Wakalenjin ni chakula kigeni. Wao kipindi cha kutafsiri Biblia ya Kikalenjin, mkate ulikuwa unajulikana kwa wachache mno. Hali hii ilipelekea mtafsri akwepe kutafsiri dhana ya mkate kwa kuwa haingebainika wazi kwa wasomaji wa
*Bukuit Ne Tilil*. Ukweli huu unatokana na tafsiri ya sehemu ifuatayo ya Biblia.

**Mfano 2.**
Mithali 9:5 **M.A**- Njoo ule mkate wangu, Ukanywe divai niliyoichanganya. **M.P**- *Nyo, am amitwogikyuk, Ak iee divaik che kaaburuch.*
Tunavyoona katika tafsiri hii ni kuwa, neno ***mkate,*** limepewa tafsiri ya ***amitwogikyuk***
(chakula changu). Mtafsiri kwa kuzingatia L.P, hangeweza kupata kisawe cha neno, Mkate, kwa kuwa Wakalenjin hawakuwa na chakula hiki. Kwa hivyo alitumia neno la jumla la 'chakula' ili kuwasilisha dhana ya mkate.

**Mfano 3.**
Mithali 23:6 **M.A**- Usile mkate wa mtu mwenye husuda; Wala usivitamani vyakula Vyake vya anasa;

**M.P**- *Ameam amitwogikabinendet netinyei kong' ne ya, Amemach amitwogikyik che anyiny:*
Neno ***mkate*** limetafsiriwa kama ***amitwogikab*** (chakula cha). Kutokana na tafsiri hizi, tunaona kuwa Wakalenjin hawakutumia mkate kama aina ya chakula, hawakuwa na chakula aina ya mkate. Ili kukwepa kutofahamika kwa neno hili, alichagua kutumia neno la jumla ambalo ni 'chakula', na hivyo kuuwasilisha ujumbe wa mwandishi wa M.A kama alivyokusudia.

**Tafsiri ya Dhana Zinazohusu Jinsia**
Wakalenjin katika mila na tamaduni zao, hutukuza jinsia ya kiume kuliko jinsia ya kike. Mwanamke huchukuliwa kama mtoto na kwa hivyo mwanamume hurejelewa katika hali mbalimbali kuliko ilivyo mwanamke. Wakati Waswahili wanatumia neno linalojumlisha jinsia zote mbili; yaani kiume na kike, hutumia neno 'mwana'. Lakini Wakalenjin wanaonekana kototambua jinsia ya kiume na badala yake huashiria jinsia ya kike.
Vifungu vinavyozingatia tafsiri hii ya 'mwana' kwa maana ya 'mtoto wa kiume' ni vingi katika kitabu hiki cha Mithali. Baadhi ya vifungu hivyo ni pamoja na:
**Mfano 4.**
Mithali 10:1 **M.A**- Mwanamwenye hekima humfurahisha babaye Bali mwana mpumbavu ni mzigo wa mamaye.
**M.P**- *Iboiboi werit ne ng'om kwanda:*
*Ago inyalili werit ne berber kamet.*
(***Werit*** kwa maana ya ***mwana wa kiume***)
Mithali 13: 1 **M.A**- Mwana mwenye hekima husikiliza mausia ya babaye; Bali mwenye dharau hasikilizi maonyo.
**M.P**- *Epchin it werit ne ng'om kotigonetab kwandanyi: Ago magasei keretab kong' chotindet.*
(***Werit*** kwa maana ya ***mwana wa kiume***)


© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Mithali 15:20 **M.A**- mwana mwenye hekima humfurahisha babaye; Bali mpumbavu humdharau mamaye.

**M.P**- *Iboiboi kwanda werit ne ng'om:*
*Ago sasei kamet chito ne berber.*
(***Werit*** kwa maana ya ***mwana wa kiume***)

Mithali 19:13 **M.A**- Mwana mpumbavu ni msiba kwa babaye; Na ugomvi wa mke kama kutona-tona daima.

**M.P**- *Nyalildab kwandandanyi werit ne berber:*
*U beek che saitoi bolatetab osotiot.*
(***Werit*** kwa maana ya ***mwana wa kiume***)

Mithali 28:7 **M.A**- Yeye aishikayesheria ni mwana mwenye hekima; Bali aliye rafiki wa walafi humwaibisha babaye.

**M.P**- *Werit ne ng'om age tugul ne ribei ng'atutik:*
*Ago itewri kwandanyi inendet ne choruetab kipkeinik.*
(***Werit*** kwa maana ya ***mwana wa kiume***)

Kwenye mifano hii hapa juu, ni dhahiri kuwa neno ***werit*** ni tafsiri ya neno mwana na ambaye katika muktadha huu wa Kikalenjin lina maana ya mwana wa jinsia ya kiume. Katika Kiswahili, neno hili halibagui jinsia bali linatumika kwa maana ya mtoto wa jinsia yoyote ile- awe wa kiume au wa kike. Lakini katika jamii ya Kikalenjin, utamaduni wao unamuenzi sana mtoto wa kiume. Hali hii inapelekea mtafsiri kulitafsiri neno hili kwa kuegemea mkondo wa kiutamaduni ambapo anapendelea mtoto la jinsia ya kiume. Iwape angetafsiri tu bila kuzingatia utamaduni wa Kikalenjin, basi tafsiri ya neno hili lingekuwa ***lakwet***, kwa maana ya mwana – yaani wa jinsia yoyote.

**Mfano 5.**

Mithali 8:32 **M.A**- Basi, wanangu, nisikilizeni sasa;
Maana heri hao wazishikao amri zangu.

**M.P**- *Ogasa anyun, werju:*
*Amu iberurotin ichek che ribei ortimwekyuk.*
(***Werju*** ina maana ya ***wana hawa wa kiume***)

Katika mfano huu hapa juu, tunaona jinsi neno wanangu linavyotafsiriwa kama ***werju***. Tafsiri hii inazingatia jinsia ya kiume na kutupilia mabli jinsia ya kike. ***Werju*** ni neno linalotumika kama kivumishi kiashiria cha karibu lakini katika wingi, linaloonyesha jinsia ya kiume wala si kike. Mwandishi wa Biblia ya Kiswahili alikusudia kuwasiliana na jinsia zote lakini mtafsiri anaegemea kwa jinsia moja.

**Taasubi ya Kiume katika Tafsiri**

Hii ni hali ambapo mwanamume anaonekana kupendelewa kuliko mwanamke, yaani, mwanamke anadunishwa. Hali kama hii huweza kutokea kwa mfano iwapo mambo mazuri yanahusishwa na wanaume ilhali mambo maovu yanahusishwa wanawake. Katika Biblia ya Kikalenjin, mtafsiri ameonyesha hali hii kwa namna ya wazi kabisa katika tafsiri yake kwa kuwahusisha wanawake na mambo hasi huku wanaume wakihusishwa na mambo chanya. Tutazame mifano hii:

**Mfano 6.**

Mitahli 2:16 **M.A**- Ili kuokoa na malaya,
Naam, malaya mwenye kubembeleza kwa maneno yake.

**M.P**- *Si gosor eng' chepkugoniot,*
*Ee, kwondo ne chemwai kut;*

Katika tafsiri hii, neno ***malaya*** ambalo kwa L.A (Kiswahili) linaashiria jinsia zote, yaani ya kike na kiume, limetafsiriwa kama ***chepkugoniot*** (mwanamke malaya). Kiambishi **'*chep*'** ikiwa ni kiwakilishi kiambishi cha nafsi ya mwanamke. Jambo la wazi ni kuwa mwanamke amedunishwa kwa kuonekana kama ndiye malaya wala si mwanaume. Msisitizo huo pia upo katika sehemu ya pili ya kifungu. M.A katika mstari unaofuata unazungumzia malaya kuwa anabembeleza, lakini M.P inazungumzia mwanamke (***kwondo***) mwenye kubembeleza kwa



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

maneno matamu (***ne chemwai kut***). Kumaanisha kuwa wanaobembeleza si wanaume bali ni wanawake.
Tunapata hali kama hii vile vile katika tafsiri ifuatayo:

**Mfano 7.**
Mithali 5:3 **M.A**- Maana midomo ya malaya hudondoza asali, Na kinywa chake ni laini kuliko mafuta:
**M.P**- *Amu saune kumiat kutitab chepkugoniot, Ago tangusen nag'alekyik kosiir mwaita:*
Katika tafsiri hii, neno ***malaya*** limetafsiriwa kama ***chepkugoniot*** (mwanamke ambaye ni malaya). Vile vile;
Isitoshe, mtafsiri wa Bibilia ya Kikalenjin anaendelea kuonyesha jinsi utamaduni wa
Wakalenjin unavyomtukuza mwanaume. Tutazame hapa chini;
**Mfano 8.**
Mithali 7:19 **M.A** Maana mume wangu hayumo nyumbani, Amekwenda safari ya mbali.
**M.P** *Amu mami ga chitab kobo got, Kawa banda ne loo:*
Katika tafsiri hii, maneno, ***mume wangu*** yametafsiriwa kama ***chitab kobo got*** (mtu mwenye kumiliki nyumba). Labda mtafsiri angetafsiri kama ***manong'otiannyu*** (mume wangu) kama ilivyowasilishwa katika M.A. Lakini kutokana na tafsiri hii, inadhihirika kuwa katika jamii ya Wakalenjin, mwanaume ndiye mwenye kumiliki nyumba wala si mwanamke. Licha ya kuwa wameoana, hawawezi kumiliki nyumba wote wawili kama jamii, ila nyumba ni mali ya mwanamume pekee. Badala ya mwanamke huyu kudai kuwa mume wake hayuko nyumbani, anasema kuhusu yule mwenye nyumba ambaye katika jamii ya wakalenjin ni mwanaume. Mwanamke kamwe hawezi kumiliki nyumba au hata mali iliyoko katika boma ambapo ameolewa.
Kazi yake ni kuzaa na kuchunga mali ya mumewe wala si kumiliki. Tafsiri hii inaonyesha jinsi Wakalenjin wanavyowatukuza wanaume huku wakiwadunisha wanawake katika utamaduni wao.

**Tafsiri Inayohusu Hali za Kimazingira**
Wakati wa kutafsiri, mtafsiri huzingatia mazingira ya walengwa huku akilinganisha na mazingira ya hadhira asilia. Endapo mazingira yao ni tofauti, ina maana kwamba lazima atakuwa makini ili kwamba awasilishe ujumbe wa M.A kwa namna ambavyo haitaathiri ujumbe asilia kwa kuwa mara ninyi, kimazingira hutofautiana kutoka kwa jamii hadi nyingine. Katika kutafsiri Biblia ya Kiswahili hadi Kikalenjin, ni bayana kuwa mazingira ya Waswahili ni ya pwani huku ya Wakalenjin yakiwa ni ya bara. Mtafsiri hivyo basi hulazimika kuzingatia hali hii na hivyo kufanikisha mawasiliano ya mwandishi wa M.A kwa H.P. Katika Biblia ya Kikalenjin, tunaona namna mtafsiri alivyokabiliana na hali hizo kwa namna ya kipekee. Kwa mfano katika tafsiri ifuatayo;

**Mfano 9.**
Mithali 20:17 **M.A** Chakula cha uongo ni kitamu kwa mtu; Lakini halafu kinywa chake kitajaa changarawe.
**M.A** *Anyiny eng' chi amitwogikab lembeita; Ago ne matia konyi kutinnyi koik.*
Changarawe ni aina ya mchanga unaopatikana kando kando mwa bahari, maziwa au hata mito. Ni aina ya mchanga uanotumika sana katika ujenzi wala si bora sana katika ukulima wa nafaka nyingi. Mchanga aina hii haupatikani sehemu nyingi za bara. Wakalenjin ni wafugaji na kwa hiyo walipendelea maeneo yenye malisho bora kwa mifugo yao ambapo, hasa ni sehemu za bara. Waswahili walijihusisha katika biashara na uvuvi na hivyo wao ni watu wanaopatikana katika pwani ya Kenya. Kutokana na kuwepo kwa Bahari ya Hindi, sehemu ya pwani basi ina wingi wa changarawe.

Katika tafsiri ya kifungu hiki hapo juu, mtafsiri alitafsiri neno ***changarawe*** kama ***koik*** (mawe). Hii ni kwa sababu



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

H.P ambao ni Wakalenjin hawangeelewa changarawe kwa sababu ya kuishi katika mazingira yasiokuwa na mchanga aina hii. Ukulima wa mimea kama mahindi na mtama uliokuwa maarufu miongoni mwa Wakalenjin na hauwezi ukafanyika sehemu yenye mawe. Kwa hiyo ili kuleta picha ya ukavu unaotokana na changarawe, mtafsiri alitumia neno mawe ili kufanikisha mawasiliano yake na H.P.

**Tafsiri ya Mila na Desturi**

Wakalenjin wana mila na desturi zao ambazo ni tofauti na zile za Waswahili. Hali hii inafaa kuzingatiwa wakati wa kutafsiri matini moja kwenda kwa nyengine ili mwishowe, kuwe na welewa kwa wanaokusudiwa na kazi tafsiri. Katika kutafsiri Biblia ya Kiswahili kwenda kwa lugha ya Kikalenjin, tunaona mtafsiri akizingatia hoja hii.

**Mfano 10.**

Mithali 24:11 **M.A** Uwaokoe wanaochukuliwa ili wauawe;
Nao walio tayari kuchinjwa uwaopoe.
**M.P** *Soru ichek che kimuti koba meet,*
*Ak iet ichek che kimachei kebar.*

Katika kutafsiri sehemu hii, mtafsiri ametafsiri neno ***kuchinjwa*** kama ***kebar*** (kuuawa). Wakalenjin katika desturi na mila zao, mwanadamu hachinjwi (keeny) ila ni mnyama tu ambaye huchinjwa. Mwanadamu huwawa (***kebar***), kwa sababu mwanadamu ndiye anayeaminika kuwa na nafsi tofauti na aliyonayo mnyama. Kwa hiyo katika kutafsiri kwa namna ambavyo ujumbe wa mwandishi wa M.A ungeweza kuhifadhiwa, basi ilimpasa mtafsiri kuzingatia mila na desturi za Wakalenjin na kuwasiliana kwa urahisi. Katika mila ya Wakalenjin, mnyama huchinjwa kwa minajili ya kuliwa nyama. Hii ndio sababu, mtafsiri hangeweza kutafsiri vivyo hivyo kwa sababu mwanadamu katika jamii ya Wakalenjin haliwi kama alivyo mnyama. Iwapo mtu atauliwa, ina maana kuwa hawezi akaliwa lakini kama atachinjwa, ina maana kuwa ataliwa; jambo ambalo si la kawaida katika mila na desturi za Wakalenjin.

**Mfano 11.**

Mithali 15:17 **M.A** Chakula cha mboga penye mapendano;
Ni bora kuliko ng'ombe aliyenona pamoja na kuchukiana.
**M.P** *Kaigai keam ngwek eng' ole mi chamnyet,*
*Kosir eito ne akwai koboto wechet.*

Mtafsiri hapa ameonyesha jinsi desturi ya Wakalenjin ilivyo. Anapotafsiri ***ng'ombe*** kama ***eito*** (ng'ombe dume), anatuonyesha bayana kwamba Mkalenjin hawezi kumchinja ng'ombe wa kike kwa ajili ya kuliwa kama chakula ila dume ndiye huchaguliwa. Wakati wa sherehe au kama kuna haja ya kutumia nyama kama chakula, Wakalenjin huchagua ng'ombe dume pekee kwa kazi hiyo. Hiyo ndiyo sababu hali hii inaonekana katika tafsiri hii.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### Hitimisho

Katika sura hii tumeoana vipengele kadha wa kadha vinavyohusiana na utamaduni wa jamii ya Wakalenjin na jinsi vipengele hivyo vilivyozingatiwa katika kutafsiri Biblia ya Kikalenjin (*Bukuit ne Tilil*) ili kukuza ujumbe wa mwandishi wa M.A, huku ujumbe wa M.A ukiwasilishwa kwa namna ambayo H.P hufikiwa. Utamaduni ni jambo la muhimu sana katika jamii yoyote ikiwemo jamii ya Wakalenjin.

Hii inapelekea mtafsiri kuwa makini sana anapotafsiri dhana za kitamaduni. Nadharia ya tafsiri vitendo imebainisha wazi kuwa kuwa tamaduni zote ulimwenguni hazifanani, na kwa hivyo mtafsiri anapaswa kuelewa utamaduni wa H.A na ule wa H.P, ili anapotafsiri, aweze kuchagua kwa makini msamiati mwafaka wa kutumia



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

katika M.T, na hivyo kusababisha H.P kuelewa ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa M.A. Kutokana na uchunguzi huu tumeona kuwa mtafsiri alibadilisha vipengele mbalimbali vilivyowasilishwa katika M.A, ili viweze kukimu mahitaji ya kitamaduni ya H.P.

Haya yanaafiki maelezo ya nadharia ya ulinganifu sambamba ambayo yanapendekeza vipengele vya kitamaduni vidabadilishwa ili kuafiki matakwa ya utamaduni wa lugha pokezi, kwa sababu utamaduni wa Wakalenjin ni tofauti na ule wa Waswahili. Ili kuwafikia Wakalenjin, ilimpasa mtafsiri kuzingatia utamaduni wa Wakalenjin na hivyo kuwafanya waone kuwa M.P inawalenga wao wenyewe. Uandishi upya umetekelezwa hapa na mtafsiri ili kuhakikisha kuwa H.P inapokea ujumbe wa mwandishi wa M.A pamoja na athari sawa na za H.A, kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri vitendo. Tofauti za kitamaduni pia zimechangia kwa mtafsiri kuandika upya M.L ili wasomaji ambao ni Wakalenjin, wanapoisoma, wataona kama ni kazi halisi wala haijatolewa kwingineko. Uandishi upya pia umesaidia M.L kueleweka vyema kwa H.P, kwani kama ingelitafsiriwa tu moja kwa moja bila kubadilisha dhana yoyote ili kukidhi mahitaji ya Wakalenjin, basi tafsiri hii haingeweza kuhifadhi ujumbe wa mwandishi wa M.A na hivyo kupotosha H.P. Kijumla, nadharia hizi mbili zilikuwa muhala katika kutafsiri vipengele vya kitamaduni katika *Bukuit Ne Tilil.* **Mapendekezo**Sera za elimu kuhusiana na lugha za kienyeji zinafaa kutiliwa maanani ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata kuzielewa lugha zao za kienyeji. Jambo hili litahakikisha kuwa kazi zinazotafsiriwa hadi lugha za kienyeji zinapata wasomaji, la sivyo, ujumbe wa matini hizi hazitapata wasomaji wengi.

## MAREJELEO

Agar, M. (1994). *Language Shock: Understanding the Culture of Conversation.* Cambridge: Cambridge University Press

Alvarez, R. R., & Vidal, M.C.A. (1996). "Translating: A Political Act". *Translation Power Subversion.* Clevedon: Multilingual Matters Ltd.

Baker, M. (1992). *In Other Words: A Coursebook on Translation.*London: Routledge. Bassnett, S. (1980). *Translation Studies.* London: Routledge.

Biamah, J. (2012). *Methods and Trends of Interpretation.*Deutschland: Lambert Academic Publishing.

Bryson, S. M. (1959). *The History of the Nandi People; Light in Darkness.* England: Parry Jackman.

Buliba, A. F. (2001). "Lugha, Utamaduni na Jamii, katika Maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa" katika Shitemi N.L na wenzake (2001). *Kiswahili A Tool for Development the Multidisciplinary Approach*. Eldoret: Moi University press.

Catford, J. (1965). *A Linguistic Theory of Translation.*New York: Oxford University Press. Hatim, B., & Mason, I. (1994). *Discourse and the Translator.*New York: Longman.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili., Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Harvey, M. (2012). "A beginner's course in Legal Translation: The case of CultureboundTerms". Katika A.F. Guerra (2012). "Translating Culture Problems, Strategies and Practical realities" Juzuu la *Literature, Culture and Literary Translation.*

Hongwei, C. (1999). *Cultural Differences and Translation.* Wuhan: central China Normal University

House, J. (2009). *Translation.* Oxford: Oxford University Press.

Katan, D. (1999). *Translating Culture an Introduction for Translators, Interpreters and*

Kramsch, C. (1998). *Language and Culture*. New York: Oxford University Press

Krings, H.P. (1986). "Translation Problems and Translation Strategies of Advance German Learners of French" katika J, House na S.Blum-Kulka (Whr), *Interlingual an Intercultural Communication.* UK. 263-26. Tubingen: Gunterman.

Larson, M. (1984). *Meaning-Based translation: A Guide To Cross-Language Equivalance* (2nd Ed) New York & London: Un. Press of America

Lefevere, A. (1992). *Translation, Rewriting and the Manipulation of Literary Fame* London/ New York: Routledge.

Lefevere, A. (1999). "Mother Courage's Cucumber: A Text, System and Refraction in a Theory of Literature".Katika Venuti, L. (mhr). *The Translation Studies Reader.*London: Routledge.

Mish, J. L. (1988). "The World as language". Katika Newmark. *Approaches to Translation.* Upper Saddle River: Prentice Hall.

Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies, Theories and Application.* London na New York: Routledge.

Newmark, P. (1988). *Approaches to Translation.*Cambridge: Cambridge University Press.

Nida, A.E. (1988). "Translation as Communication". Katika Newmark. *Approaches to Translation* Upper Saddle Rive: Prentice Hall.

Nida, E.A., & De Waard. (1986). *From One Language to Another: Functional Equivalence in Bible Translating.* Nashvill: Thomas Nelson Publishers.

Nida, E.A., & Taber. (1969). *The Theory and Practice of Translation.* Leiden: Brill.

Ogechi, N. O. (2002). *Mbinu za Mawasiliano kwa Kiswahili.* Nairobi. FotoForm Ltd.

Pym, A. (1995). *Translation as Transaction Cost.* Frankfurt: Peter Lang.

Salehi, M. (2012). "Reflections on Culture, Language and Translation" Katika *The Journal of Academic and Applied Studies*. Juzuu.2 (5). Uk 76-85.

Sapir, E. (1949). *Culture, Language and Personality*. London: University of California Press

Shitemi, N. L. (1997). *Uaminifu katika Tafsiri za Ushairi wa Jadi wa Kiswahili. Utenzi wa Inkishafi, Utenzi wa mwanakupona na Mashairi ya Muyaka.* Tasnifu: Dphil.Eldoret, Moi University. (Haijachapishwa).

Shitemi, N. L. (2001). "Language as a Tool for development: Issues to Ponder" katika, Shitemi, N. L., na wenzake (2001) *Kiswahili A Tool for Development the Multidisciplinary Approach*. Eldoret:Moi University press.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Snell-Hornby M. (1988). *Translation Studies: An Integrated Approach*. America: John Publishing Company

Sun, H. (2011). "On Cultural Differences and Translation Methods" Katika Jarida la *Language Teaching and Research*. Juzuu 2 uk. 160-163. Finland: Academy Publishers

Toury, G. (2012). *Descriptive Translation Studies and Beyond.* John Benjamin Publishing.

Venuti, L. (1998). Strategies of Translation Katika M. Baker (Mhr) *Encyclopedia of Translation Studies.* (Uk. 240-244).London and New York: Routledge.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org